**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!...**
Napenda nianze kwa kuupongeza uongozi wa CTI kwa kuandaa shindano na hafla hii ya Utoaji wa Tuzo za Rais kwa Wazalishaji Bora (*President's Manufacturer of the Year Awards – PMAYA*) kwa mwaka 2023. Aidha, ninatoa shukrani za dhati kwa CTI na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kumualika Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgeni Rasmi katika Hafla hii. Licha ya kuridhia, Mhe. Rais hakuweza kujumuika nanyi, kutokana na majukumu mengi ya kitaifa aliyonayo na hivyo amenipa tena heshima ya kumwakilisha kama ilivyokuwa mwaka 2021 na 2022. Mhe. Rais anatambua na kuthamini jitihada za Wazalishaji wa bidhaa za viwandani na kupitia Falsafa yake ya R4 ametilia mkazo ajenda ya mageuzi ya viwanda na kuelekeza izingatiwe katika mipango ya maendeleo ya Taifa. Pia, anawashukuru sana wenye viwanda kwa kuunga mkono na kuwezesha utekelezaji wa ajenda yake ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini, ili kufikia lengo la 80% ya kaya zote kutumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2034. Aidha, anapongeza sana ushirikiano mzuri uliopo baina ya Serikali na Wazalishaji wa bidhaa za viwandani na kwa mchango mkubwa mnaotoa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***
Hafla hii ni fursa adhimu ya kutambua na kuwatunuku wazalishaji wa bidhaa za viwandani wanaoonesha uvumbuzi uliotukuka na kuongeza tija, ubora wa hali ya juu wa bidhaa wanazozalisha, na dhamiri thabiti ya kuendeleza viwanda nchini. Aidha, tukio hili ni fursa nyingine ya kujenga mahusiano na kubadilishana mawazo kati ya wazalishaji wa bidhaa za viwandani na watoa huduma wa ndani. Natumaini kuwa hafla hii inatumika pia kutambua wazalishaji viwandani wanaofanya vizuri zaidi kwa ushirikishwaji mzuri wa wafanyakazi kufikia malengo ya uzalishaji.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***
Sekta ya viwanda ni moja ya sekta za uzalishaji hapa nchini, zenye uwezo mkubwa wa kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi. Duniani kote, sekta ya viwanda ndiyo chimbuko la maendeleo ya haraka katika nchi. Kwa maneno mengine sekta hii ina fursa kubwa ya kukua haraka, kutengeneza fursa za ajira na pia kuchochea ubunifu na maendeleo ya kiteknolojia. Vilevile, ni sekta yenye uwezo wa kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi na hivyo kuliletea Taifa fedha za kigeni. Sekta ya viwanda pia ina mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta nyingine *(forward and backward linkages)*. Hata hivyo, licha ya nafasi kubwa ya sekta ya viwanda kuchangia zaidi katika ukuaji wa pato la Taifa, mchango wa sekta ya viwanda hapa nchini bado ni mdogo (8.1% ya pato la Taifa) na wastani wa ukuaji wake ni 8% kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita. Mapato ya fedha za kigeni kutokana na mapato ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 0.9 bilioni mwaka 2020 hadi Dola za Marekani 1.4 bilioni mwaka 2023 lakini inaweza kutuingizia zaidi. Vivyo hivyo, mchango wa sekta ya viwanda kwenye ajira rasmi unakadiriwa kuwa 12.2% kwa 2023. Baadhi ya changamoto zinazozuia maendeleo ya haraka ya sekta ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani ni pamoja na ugumu wa kupata mitaji ya gharama nafuu, uhaba wa rasilimaliwatu yenye ujuzi, utafiti na maendeleo usiojitosheleza, matumizi ya teknolojia

zilizopitwa na wakati na zenye tija ndogo, miundombinu isiyokidhi mahitaji hususan ya nishati na usafirishaji pamoja na vikwazo visivyo vya kikodi. Ili kukabiliana na changamoto hizo, zinahitajika jitihada za pamoja za wadau ili kuhuisha ubunifu, kuongeza tija na kutegemeza ushindani wa sekta ya viwanda.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Kama mnavyofahamu, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha viwanda vyetu vinakuwa katika mazingira wezeshi yanayoweza kuchochea ufanisi na ushindani katika masoko. Serikali inafanya jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi zinazojumuisha kuimarisha usafiri wa anga na reli ambapo hadi sasa reli ya kisasa ya mwendokasi (SGR) kutoka Dar es salaam kwenda Dodoma imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa abiria. Pia, ujenzi wa Bandari Kavu ya Ihumwa, Dodoma unaendelea, pamoja na kujenga vipande vilivyosalia vya reli hadi kufika Mwanza na Kigoma. Hii inaenda sambamba na upanuzi na uboreshaji wa utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kurahisisha upakiaji na utoaji wa mizigo kwa haraka. Aidha, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere –JNHPP (99.21%). Hadi sasa, takriban MW 1,175 zimeingizwa katika Gridi ya Taifa ambapo uzalishaji wa umeme nchini sasa umefikia MW 3,077.96. Vilevile, Serikali inaendelea na usambazaji wa umeme vijijini ili kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanafikiwa na huduma hiyo ili kuwezesha uwekezaji na uzalishaji. Serikali pia imefikia hatua nzuri katika ujenzi wa kongani za viwanda, ikiwemo Kongani ya Viwanda ya Kwala, Kongani ya Kisasa ya Viwanda (*Modern Industrial Park*) ya Mlandizi, na Ujenzi wa Miundombinu ya Msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO, Kibaha. Aidha, kama ilivyoelezwa tayari, Wizara ya viwanda na biashara inakamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika. Lengo ni kuongeza wigo wa soko kwa Wazalishaji wa bidhaa za viwandani na Wafanyabiashara kwa ujumla.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Hatua nilizozitaja, zimeiwezesha Tanzania kuwa eneo salama kwa uwekezaji na kuimarisha uchumi. Kulingana na tathmini ya WB kuhusu mazingira ya biashara na uwekezaji (*World Bank Group Business Ready Report, 2024*), Tanzania ni nchi ya tano kati ya nchi 50 duniani za kipato cha chini na kipato cha kati (ngazi ya juu na ya chini), kwa ufanisi na utoaji wa huduma bora za umeme, huduma za mtandao/internet na huduma nyingine. Aidha, tathmini ya taasisi ya *Moody's* hivi karibuni iliipatia nchi yetu, alama ya B1 yenye mwelekeo imara, kutoka alama B2 mwaka 2022. Kadhalika, mwezi Desemba 2023, taasisi ya *Fitch*, ilitoa alama ya B+ kwa Tanzania. Matokeo ya tathmini hizi ni ishara ya kuimarika kwa uchumi wetu na uwezo wa nchi kukopesheka.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Kama mnavyofahamu, Serikali kwa kushirikiana na wadau, iko katika hatua ya kuandaa Dira ya Taifa 2050 baada ya kukusanya maoni ya makundi mbalimbali ya jamii yetu kuhusu Tanzania wanayoitamani ifikapo mwaka 2050. Inaonekana Watanzania wengi wanatamani mabadiliko makubwa kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya kipato cha kati, daraja la juu kama tutajipanga vizuri kutumia rasilimali nyingi tulizojaliwa kama Taifa. Aidha, tunatambua kwamba uchumi wa dunia unapitia mabadiliko makubwa yanayotokana na siasa za kikanda

(*geopolitics*), mabadiliko ya haraka na makubwa ya kiteknolojia, ushindani mkali, mabadiliko ya tabianchi na mabadiliko ya kijamii kwa ujumla. Kwa hiyo, wakati Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua changamoto zinazoathiri ukuaji wa Sekta ya Viwanda, ni muhimu pia wazalishaji viwandani wakatambua wajibu wao katika kufikia shauku ya Watanzania ifikapo 2050, na kujenga uhimilivu *(resilience)* dhidi ya changamoto hizo za kidunia. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kusisitiza yafuatayo:

**Kwanza**, ninatoa rai kwa CTI kubainisha sekta, sekta ndogo na viwanda zinavyokua haraka *(most dynamic)* ambavyo tayari zimefanikiwa kujipenyeza katika masoko ya kikanda na kimataifa ili kubaini nini kinachohitajika kushughulikiwa na sekta binafsi au Serikali au kwa ubia, kuviwezesha viwanda hivyo viweze kuongeza tija, uzalishaji na mauzo kama sehemu ya mkakati wa kufikia ndoto za Watanzania 2050. Aidha, nawaomba wenye viwanda kubuni mikakati ya kujihami dhidi ya athari zinazotokana na dhoruba katika uchumi wa dunia *(build resilience to global shocks)*. Vilevile, ninawasihi wazalishaji wa bidhaa za viwandani kuchukua hatua zaidi kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za uzalishaji wao, ikiwa ni pamoja na urejelezaji wa taka ngumu kama plastiki *(recycling)* kama zilivyofanya baadhi ya Kampuni za usindikaji wa vinywaji baridi.

**Pili,** natoa rai kwenu kuongeza wigo wa uwekezaji katika viwanda mbalimbali vya kimkakati. Hivi sasa, tunafanya vizuri kiasi, katika viwanda vya kuzalisha bidhaa za walaji *(consumer goods),* vinywaji *(beverages)*, vyakula (hasa uchakataji wa unga wa ngano), bidhaa za ujenzi hususan saruji, nondo, marumaru na mabati. Hata hivyo, viwanda vya aina hii bado vinategemea sehemu kubwa ya malighafi zake kutoka nje. Naamini kuwa wakati umefika sasa wa kuvipa uzito viwanda vinavyozalisha bidhaa za kati *(intermediate goods industries)* hususan vile vinavyozalisha ajira kwa wingi, kuchochea ubunifu, tija na vyenye uhusiano mkubwa na sekta nyingine *(forward and backward linkages)*.

**Tatu,** natoa wito kwa Wazalishaji wa bidhaa za viwandani, na Sekta Binafsi kwa ujumla, kutumia nguvukazi kubwa ya vijana tuliyonayo. Nashauri muanze kwa kuwapatia vijana fursa zaidi za mafunzo ya vitendo kazini *(internship/field attachment)* ili kuongeza ujuzi wao na kuwadhamini. Aidha, Serikali kwa upande wake imeanza kufanya mageuzi makubwa ya mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo ya amali ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira, mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia.

**Nne**, ninapenda kuwasisitiza wazalishaji wa bidhaa za viwandani kuingia ubia na wadau wengine (kutoka ndani na nje ya nchi) ili kuanzisha vituo atamizi vya sayansi, teknolojia na uvumbuzi (*technology incubation centers*) ili kulea na kuasili teknolojia zinazochipukia (*nurturing technology start-ups*). Hili ni muhimu kwani litasaidia kuhawilisha teknolojia na kuwaunganisha wavumbuzi wa teknolojia duniani na wazalishaji wa bidhaa za viwanda nchini.

**Tano,** taarifa zilizopo zinaonesha kuwa kuna uagizaji holela wa bidhaa za viwandani kutoka nje. Kwa mfano, katika 2023/24, jumla ya bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 9 ziliteketezwa na taasisi husika za Serikali kutokana na kukosa ubora. Bidhaa hizo ni pamoja na bidhaa za chakula zenye thamani ya shilingi bilioni 4.7; bidhaa za vipodozi zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6; mitumba ya nguo za ndani *(undergarments)* yenye thamani ya shilingi

milioni 30.4; bidhaa za ujenzi (mabati na saruji) zenye thamani ya shilingi bilioni 2.3; na bidhaa za kemikali zenye thamani ya shilingi milioni 468.2. Kwa maoni yangu, tatizo hili ni fursa kwa wazalishaji wa bidhaa za viwandani hapa nchini, kuongeza uzalishaji katika maeneo haya ili kukidhi mahitaji ya ndani, sambamba na jitihada za Serikali kudhibiti uingizwaji wa bidhaa zisizokidhi ubora.

Aidha, ninatambua jitihada mbalimbali zinazofanyika kutangaza bidhaa zetu za ndani hususan kupitia maonesho kama vile Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es salaam *(Dar es salaam International Trade Fair)* yanayofanyika mwezi Julai kila mwaka, na Maonesho ya kimataifa ya bidhaa za viwandani *(Tanzania International Manufacturers EXPO)* yaliyofanyika mwezi Septemba 2024. Ninaitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na CTI na wadau wengine kuendeleza jitihada hizo na kupanua wigo wa kukuza na kutangaza bidhaa zetu, ndani na nje ya nchi.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Mwisho, napenda kuwapongeza na kuwashukuru waandaaji, washiriki wa shindano la mwaka 2023 na wadhamini wa tukio hili, hususan TPA, TRA, Alliance Life Insurance Ltd, ALAF Ltd, TCC Plc, Motisun Group Ltd, Plasco Ltd, Kilimanjaro Cables Ltd, Azam Media, Mati Super Brands Ltd, Serengeti Breweries Ltd, Tanzania Breweries Ltd, Bonite Bottlers Ltd pamoja na wengine wote waliochangia kwa namna mbalimbali.

Baada ya kusema hayo, naomba nihitimishe hotuba yangu ili tuweze kuwatambua Washindi wa Tuzo za Rais ya Wazalishaji Bora wa Viwandani kwa Mwaka 2023. Natanguliza pongezi za dhati kwa washindi wote na kwa wale ambao sifa hazikutosha, nawahimiza waongeze bidii ili waweze kushinda mwakani.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**